MIMI NA WENGINE

MEAND OTHERS

































I YOU SHE HE IT THEY WE YOU





Mimi (I)



Mimi ni Emma.

Mimi nina miaka sita

Mimi ninasoma darasa la kwanza

Mimi ninajua kusoma

Mimi ni mwanafunzi.

I am Emma

l am six years old

I am in grade one

I know how to read

I am a student

VVEWE (YOU) SINGULAR



Wewe ni mwalimu

Wewe una miaka ishirini

Wewe unafundisha hesabu

Wewe unafanya kazi nzuri

Wewe una darasa kubwa

You are a teacher


You are 20 years old

You teach math

You do a great job

You have a big class

Yeye (She/He/It)



Yeye ni daktari

Yeye anafanya kazi hospitali

Yeye anatibu wagonjwa

Yeye anajali wagonjwa

Yeye ni hodari sana

She is a doctor

She works at the hospital

She cures patients

She carer for patients

She is so brave

Wao (They)



Wao ni wakulima

Wao wana bustani ya mboga

Wao wanalima nyanya

Wao wanafanya kazi shambani

Wao wanapenda kilimo

They are farmers

They have a vegetable garden

They grow tomatoes

They work at the farm

They love farming

Sisi (We)



Sisi ni Madereva

Sisi tunaendesha mabasi

Sisi tunapeleka wanafunzi shuleni

Sisi tunafanya kazi kwa bidii

Sisi tunaenda kazini kila siku

We are drivers

We drive buses

We bring kids to school

We work hard

We go to work everyday

Ninyi, Nyinyi (YOU)



Ninyi ni waimbaji

Ninyi mnaimba nyimbo nzuri

Ninyi mnajua kuucheza

Ninyi mnapiga ngoma pia

Ninyi mnaimba nyimbo za kiswahili

You are singers

You sing beautiful songs

You know how to dance


You play drums too

You sing swahili songs

Mimi (I)



VVevve (YOU) SINGULAR



Mimi ni Simba

Mimi ni mfalme wa mwitu

Mimi nina rangi ya dhahabu

Mimi ninna macho makalli

Mimi ni mnyama wa porini

l am a lion

I am the king of the jungle

I am gold in color

I have sharp eyes

I am am a wild animal

Wewe ni paka

Wewe unaishi nyumbani

Wewe unapenda maziwa

Wewe una uso wa duara

Wewe ni mnyama wa nyumbani

You are a cat

You live in the house

You like milk

You have a round face

You are a pet

Yeye (It)



Yeye ni tembo

Yeye ana masikio makubwa

Yeye ana pembe ndefu

Yeye ana nguvu sana

Yeye ni mnyama wa porini

It is an elephant

It has big ears

It has long tusks

It is very strong

It is a wild animal

Wao (They)



Wao ni twiga

Wao wana madoa ya kahawia

Wao wana shingo ndefu

Wao wanatembea kwa maringo

Wao ni wanyama warembo

They are giraffes

They have brown dots

They have a long neck

They walk majestically

They are elegant animals

Sisi (We)



Sisi ni kasuku

Sisi tunapenda kuiga Sauti

Sisi tunaongea kama watu

Sisi tuna rangi za kuvutia

Sisi ni Wasema kweli

We are parrots


We like to imitate voices

We speak like people

We have beautiful colours

We are truth tellers

Nyinyi (You) Plural



Nyinyi ni nyani

Nyinyi mnaruka juu

Nyinyi mnapanda mtini

Nyinyi mnapenda kula ndizi

Nyinyi ni rafiki wa watalii

You are monkeys

You are jumping high

You are climbing a tree

You like eating bananas

You are tourists' friends

Mimi (I)



Mimi ni rubani

Mimi nina miaka thelathini

Mimi ninarusha ndege

Mimi ninatoka Arusha kwenda Mwanza

Mimi ni jasiri

I am a pilot

I am 30 years old

I fly airplanes

I am coming from Arusha to Mwanza

I am brave

Wewe (You)



Wewe ni Waziri Mkuu

Wewe ni kiongozi wa juu Canada

Wewe unaongoza wananchi

Wewe una ofisi kubwa

Wewe una watoto watatu

You are a Prime Minister

You are Canada's top leader

You lead citizens

You have a big office

You have three children

Yeye (He/She)



Yeye ni mcheza kikapu

Yeye ni mrefu sana

Yeye anakimbia haraka

Yeye anaruka juu

Yeye anafunga goli

He is a basket ball player

He is very tall

He is running fast

He is jumping high

He is scoring a goal

Wao ni polisi

Wao wanavaa sare

Wao wanalinda watu

Wao wanamkamata mwizi

Wao wanafanya kazi nzuri

They are police

Wao (They)

They wear uniform

They protect people

They are arresting a thief

They are doing a great job

Sisi (We)



Nyie (You) Plural



Sisi ni wazazi wenu

Sisi ni baba na mama yenu

Sisi tuna watoto wawili

Sisi tunapenda kusoma vitabu

Sisi tunapenda kuandika pia

We are your parents

We are your dad and mom

We have two children

We love reading books

We love writing too

Nyie ni watalii

Nyie mnapenda kusafiri

Nyie mnajifunza kiswahili

Nyie mnapanda mlima Kilimanjaro

Nyie mnaenda Ngorongoro pia

You are tourists

You love traveling

You are learning Swahili

You are climbing Mt. Kilimanjaro

You are going to Ngorongoro too

Personal Pronouns Summary



Note for Non-Swahili Speakers

This book teaches learners how to talk about themselves and others. It introduces the personal pronouns in a simplified way, while also teaching the verbs to be (ni), to have (kuwa na), to do (kufanya) and to go (kwenda) etc in correspondence with each personal pronoun.

In the end, learners can answer the questions such as: who is this/Who are they?(Huyu ni nani? Hawa ni nani?) what do they have? (Yeye ana nini? Wao wana nini?); Where are they going? (Yeye anaenda wapi? /Wao wanaenda wapi?); and what are they doing (Yeye anafanya nini/ wao wanafanya nini?). Pay particular attention to the grammatical markers below:

Kuwa Na (To have)

Mimi - Nina Sisi - Tuna NI----TU

Wewe - Una Nyinyi/Ninyi/Nyie- Mna U-----M

Yeye - Ana Wao - Wana A-----WA

Would you like to receive more kidfriendly Swahili learning resources? Sign up on the link below to be added to our mailing list:

https://mailchi.mp/9846d677d62a/swahilihome

Your feedback is important to us. To help us improve our future offerings please share your child/students' experience with this resources by contacting:

KiswahiliOttawa@gmail.com